

HOTUBA YA MGENI RASMI MHESHIMIWA DKT. SAADA MKUYA SALUM, WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS IKULU, AMBAYE PIA NI KAIMU WAZIRI WA AFYA ZANZIBAR WAKATI WA SEMINA YA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA KWA WAJUMBE WA BARAZA LA VYAMA VYA SIASA KUHUSU MPANGO WA BIMA YA AFYA KWA WOTE TAREHE 5 SEPTEMBER, 2026

Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa,

Msajili wa Vyama vya Siasa, Mhe. Jaji Francis Mutungi,

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Dr. Irene Isaka,

Viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,

Wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa,

Watendaji kutoka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa,

Watendaji kutoka NHIF,

Waandishi wa Habari,

Ndugu Wananchi,

Mabibi na Mabwana.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma, kwa kutujalia afya na kutuwezesha kukutana hapa leo katika semina hii muhimu inayolenga kujenga uelewa na kuongeza ushiriki wa wadau mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

Aidha, napenda kuushukuru Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kuandaa semina hii inayowakutanisha wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa. Ni hatua muhimu kwa sababu afya ni jambo linalomhusu kila mwananchi, bila kujali itikadi ya kisiasa, nafasi yake katika jamii, umri, jinsia au hali yake ya kiuchumi.

- **BIMA YA AFYA NI ULINZI WA FAMILIA NA UWEKEZAJI KATIKA AFYA**

Ndugu Washiriki,

Tunapozungumzia Bima ya Afya kwa Wote, tunazungumzia zaidi ya kadi au mfumo wa kupata huduma za matibabu kupitia mfumo wa Bima ya Afya ambao ni ulinzi wa mwananchi na familia yake dhidi ya gharama kubwa za matibabu.

Mwananchi anaweza kuwa na kipato kizuri leo, lakini kesho akapata ugonjwa au akapata changamoto ya kiafya inayohitaji matibabu yenye gharama kubwa. Bila kuwa na bima ya afya, familia inaweza kulazimika kutumia akiba yake, kuuza mali au kukopa ili kugharamia matibabu.

Kwa hiyo, kujiunga na bima ya afya ni hatua ya busara ya ya kulinda uchumi wa familia lakini pia kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wowote.

Kwa kupitia viongozi wote mlioko hapa na kila mtu kwa nafasi yake, nitoe wito kwenu kulibeba hili na kuendelea kuwahamasisha wananchi wote kujiunga na wasisubiri mpaka waugue ndipo tufikirie bima ya afya. Tuchukue bima tukiwa na afya ili itusaidie pale tunapohitaji huduma.

- **TUTUMIE FURSA YA MPANGO WA BIMA YA AFYA KWA WOTE**

Serikali imeendelea kuweka mazingira ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya kwa njia endelevu na yenye kuwafikia wengi.

Hivyo, ni muhimu wananchi kupata elimu sahihi kuhusu Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, namna ya kujiunga, mafao wanayostahili kupata, vituo

vya huduma vinavyotumika na namna ya kutumia mfumo wa bima kwa usahihi.

Ndugu Washiriki,

Bima ya afya ina maana pale inapokuwa inatumika. Kwa hiyo, hatutaki tu wananchi wajiunge; tunataka pia waelewe haki na wajibu wao, wajue namna ya kutumia huduma zao na watoe mrejesho pale wanapokutana na changamoto.

Ni wajibu wetu sote kuhakikisha mwananchi anayelipia au anayenufaika na bima ya afya anapata huduma stahiki kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa.

- **NAFASI YA VYAMA VYA SIASA**

Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Ninyi mna nafasi kubwa sana katika kufanikisha Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Vyama vya siasa vina mtandao mpana kuanzia ngazi ya taifa hadi ngazi ya jamii. Viongozi na wanachama wenu wanakutana na wananchi kila siku. Hivyo, mna nafasi ya kuwa mabalozi wa elimu ya afya na bima ya afya katika jamii.

Ninawaomba mtumie majukwaa yenu kuwaelimisha wananchi kwamba: “Bima ya Afya si suala la chama; ni suala la maisha ya kila mwananchi.” na Tunapowahamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya, tunakuwa tunalinda afya zao, familia zao na uchumi wa taifa.

Nawaomba viongozi wa vyama vya siasa kuhakikisha elimu hii inawafikia wanachama wenu katika mikutano, vikao, shughuli za kijamii na majukwaa mbalimbali.

- **LISHE BORA NA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA**

Ndugu Washiriki,

Nilidokezwa kuwa semina hii pia inalenga kutoa elimu kuhusu lishe na magonjwa yasiyoambukiza, hili ni jambo muhimu kwa sababu kinga ni bora kuliko tiba.

Tunahitaji kuendelea kuelimisha wananchi kuhusu ulaji unaofaa, mazoezi, kupunguza matumizi ya vyakula na vinywaji visivyo na afya, pamoja na umuhimu wa kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara.

Magonjwa yasiyoambukiza yanaweza kuathiri familia, kupunguza nguvu kazi na kuongeza gharama za matibabu. Kwa hiyo, tunahitaji kuunganisha juhudi za kinga, elimu ya afya, bima ya afya na upatikanaji wa huduma bora.

Naomba sasa nitumie fursa hii kuwaomba sana wananchi ambao bado hawajajiunga na bima ya afya kujiunga mara moja na ujumbe wangu katika hili ni ***‘Msisubiri kuugua. Jiungeni na bima ya afya sasa’***

Kwa wale ambao tayari mmejiunga, naomba itumieni bima yenu kwa usahihi, fahamuni mafao yenu na fuateni taratibu za kupata huduma.

- **HITIMISHO**

Ndugu Washiriki,

Serikali haiwezi kufanikisha Bima ya Afya kwa Wote peke yake. Mafanikio yake yanahitaji ushirikiano wa Serikali, vyama vya siasa, wataalamu wa afya, sekta binafsi, viongozi wa dini, asasi za kiraia, vyombo vya habari na wananchi wenyewe.

Ninaamini semina hii itakuwa chachu ya kuongeza uelewa na ushiriki wa vyama vya siasa katika utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

Tujenge utamaduni ambapo kila mwananchi anaona bima ya afya kuwa sehemu muhimu ya maisha yake, kama ilivyo muhimu kuwa na chakula, makazi na elimu.

Kwa pamoja, tunaweza kujenga jamii yenye afya, yenye ulinzi wa kifedha na yenye uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

Afya ya mwananchi ni msingi wa maendeleo ya Taifa, Bima ya Afya kwa Wote ni jukumu letu sote, tushirikiane kuelimisha, kuhamasisha na kuhakikisha wananchi wanajiunga na kutumia bima ya afya kwa manufaa yao, familia zao na Taifa kwa ujumla.

Kwa heshima kubwa, natamka rasmi kwamba Semina ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa kuhusu Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote imefunguliwa rasmi.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Mungu ibariki Zanzibar.

Mungu ibariki Tanzania.

Mungu awabariki wananchi wetu.

Asanteni.